
Mnara wa simu

UCSAF ilivyokwamua mawasiliano ya wanakijiji

"Mnara unatumia sola. Umeme wa TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) umefika kijijini, lakini haujaunganishwa kwenye mnara."

Na Albano Midelo

Kwa zaidi ya miaka 20, Kijiji cha Ifinga chenye wakazi zaidi ya 4,000 kilikuwa mfano halisi wa maeneo yaliyosahaulika kwenye ramani ya mawasiliano.

Awali, kijiji hicho kilichopo katika Kata ya Matumbi, Halmashauri ya Madaba wilayani Songea katika Mkoa wa Ruvuma, kilikuwa kimya si kwa kukosa watu, bali kukosa mtandao kwa ajili ya mawasiliano ya simu.

Wananchi walitembea kati ya kilometa 15 hadi 30 kutafuta sehemu ya kupiga simu.

Katika karne hii ya mapinduzi ya viwanda, hali hiyo ilikuwa sawa na kuishi nje ya dunia lakini sasa historia mpya imeandikwa.

Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imejenga minara ya mawasiliano ambayo kwa mara ya kwanza imeifanya Ifinga kusikika.

Hata hivyo, bado yapo mapambano ya kusaka huduma bora na endelevu ambayo ni mapambano ya haki ya msingi ya mawasiliano kwa binadamu.

Changamoto ya miaka mingi

Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Ifinga, Agus Ngwira anasema, "Kwa miaka mingi Kijiji cha Ifinga kilikuwa hakina mawasiliano ya simu.

"Tulitembea kwa mguu au kukodi pikipiki hadi kilometa 30 kutafuta mtandao lakini bado unarudi kijijini bila mafanikio. Siku zinapita bila kufanya mawasiliano; ilikuwa shida kweli-kweli," anasema.

Ni umbali wa kilometa 48 kutoka Barabara Kuu ya Songea - Njombe huku Ifinga ikiwa inakabiliwa na changamoto ya miundombinu duni ya barabara.

Kijiji cha Ifinga kilijikuta kikikosa mawasiliano kwa sababu hali hiyo ilisababisha changamoto katika ujenzi wa minara na usambazaji wa umeme.

Wakati UCSAF inaweka mnara wa kwanza na Halotel na kuanza kutoa huduma, furaha ilikuwa kubwa.

Hata hivyo, matumaini hayo yalipungua baada ya kuonekana kuwa mnara huo haukuwa ukitosheleza mawasiliano ya jamii yote ya Ifinga kwa saa 24 kwa sababu ulifanya kazi kwa saa kadhaa na baadaye kuzimwa.

"Asubuhi ulikuwa unawaka saa nne, usiku unazima," Ngwira anafafanua.

"Mnara unatumia sola. Umeme wa Tanesco (Shirika la Umeme Tanzania) umefika kijijini lakini haujaunganishwa kwenye mnara," anaongeza.

Miongoni mwa watu wanaoathiriwa na hali hiyo ni pamoja na walimu na watumishi wa umma wanaosema wamekuwa wakilazimika kupanda pikipiki kilometa 48 kutafuta mawasiliano.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ifinga, Michael Msigwa anasema japokuwa kuna mwanga wa mawasiliano, bado changamoto ni kubwa.

"WhatsApp haisambai, document (nyaraka) huwezi kupakua. Kwa mambo ya utawala, lazima uende Madaba ambayo iko umbali wa kilometa 48," anasema.

Katika zama za kidijiti, serikali imewekeza kwenye mifumo ya elimu, afya, manunuzi, utumishi na usimamizi.

Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sera ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ya Serikali inataka taasisi zote kutumia mifumo hiyo.

Kwa Ifinga, mifumo inakuwa mzigo kwa sababu mtandao hauwezi kuiendesha.

"Haki ya mawasiliano ni haki ya msingi ya binadamu," Msigwa anasema na kuongeza, "Tunaomba serikali iboreshe mtandao uwe wa saa 24."

Usalama wa wananchi na dharura za afya

Ifinga inapakana na Hifadhi ya Ifinga–Ruhiji, eneo la wanyama wahamao na pia kuna majangili wanaoweza kufanya uhalifu.

Wakati mwingine, dharura hutokea usiku lakini mnara unakuwa haufanyi kazi.

"Ni vigumu hata kuita gari la wagonjwa inapotekea dharura," Ngwira anasema na kusisitiza, "Hatujisikii salama."


Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ifinga, Agus Ngwira akiwa katika eneo ulipojengwa mnara wa mawasiliano ya simu.

Hili linakwenda kinyume na wajibu wa msingi wa serikali uliowekwa Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya 2015 pamoja na jukumu la UCSAF kuhakikisha huduma za mawasiliano zinawafikia wananchi wote bila ubaguzi.

Changamoto huduma za afya

Mwenyekiti wa Kijiji, Romanus Soli anaonesha fahari kubwa kwa mradi wa zahanati ya kisasa uliogharimu zaidi ya Sh milioni 140.

"Huduma zitaanza muda si mrefu, vitanda na dawa vimeshafika," anasema.

Kwa mujibu wa Soli, wakati wa msimu wa masika, mtandao huwa wa mgawo wa saa tatu hadi saa tano kwa siku.

Anasema zahanati inahitaji mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini (GoT-HoMIS) katika kutoa huduma, kusajili na kuhifadhi taarifa za wagonjwa.

Mfumo huo hauwezi kufanya kazi bila kuwapo mtandao wa uhakika wa intaneti.

Huduma za kifedha

Kuhusu huduma za kifedha, bado changamoto ni kubwa zaidi.

Wakala wa Halopesa Ifinga, Paulina Mutras anasema, "Mteja akitoa fedha, ujumbe haurejei kwa sababu mtandao unakatika. Yeye anaona fedha zimekatwa lakini mimi sijaona 'message' (arafa). Unashindwa kumhudumia."

Anasema hiyo si tu changamoto kibiashara, bali pia kwa usalama wa fedha na imani ya wananchi katika mifumo ya kidijiti.

Aidha, anasema hali hiyo husababisha baadhi ya wateja wanaonunua vifurushi kupoteza fedha zao na kupata hasara.

"Unaunga kifurushi cha wiki lakini mtandao unakaa wiki nzima umekata. Kifurushi kiki-expire (kikiisha muda wake wa matumizi) unatakiwa kuanza upya…" anasema.

Ushauri kwa serikali

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Matumbi, Yusuf Masawe anasema kwa kiasi kikubwa hali imebadilika ikilinganishwa na zamani ingawa bado kuna changamoto zinazohitaji utatuzi.

"Awali tulitembea umbali mrefu kutoa hela au kupiga simu. Sasa hali imeboreshwa lakini bado tunahitaji umeme wa Tanesco ufike kwenye minara," anasisitiza.

Kwa mujibu wa UCSAF, zaidi ya vijiji 1,000 nchini vimepata minara mipya katika miaka ya hivi karibuni lakini bado maeneo mengi hutumia nishati ya jua ambayo huwa na changamoto za uwezo na udhibiti wa umeme muda wa usiku.

UCSAF ilianza kutekeleza Mradi wa Awamu ya Kumi katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 wenye kata 280 zenye vijiji 347 kwa kujenga minara 268.

Ujenzi wa minara hiyo utakapokamilika, unatarajiwa kunufaisha wananchi zaidi ya 3,731,310 kwa huduma za uhakika za mawasiliano ya simu.

Mawasiliano ni haki

Sera ya Tehama ya Taifa ya Mwaka 2016 inataka kuwapo upatikanaji sawa wa huduma za mawasiliano kwa Watanzania wote.

Sera hiyo inasisitiza mawasiliano kuwa nyenzo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mahitaji zaidi

Kijiji cha Ifinga kimeanza kuamka na kusikika. Mnara umebadilisha maisha; umefungua milango ya mawasiliano, biashara na usalama lakini hata hivyo, bado kuna safari ndefu kuelekea kwenye mawasiliano ya uhakika.

Haya ni maweasiliano ya saa 24 yanayoweza kuendesha mifumo ya serikali, kusaidia dharura za kiafya na kulinda maisha ya watu wanaoishi jirani na hifadhi.

Wananchi wa Ifinga wanaishukuru serikali kupitia UCSAF kwa kuwafikisha katika hatua hiyo muhimu.

Hata hivyo wanasema, sauti yao bado inahitaji kusikika zaidi.

Mmoja wa wakazi wa Ifinga ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini anasema, "Tuleteeni umeme kwenye minara, tuwe sehemu ya dunia iliyounganishwa saa 24."